x. Kujisaidia eneo lisiloruhusiwa. Mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tshs. 20,000/= na kuamriwa kusafisha eneo husika.

Muhuri wa Serikali ya kijiji uligongwa kwenye sheria ndogo hizi kufuatia azimio la mkutano mkuu wa kijiji uliofanyika tarehe 11/03/2018 na muhuri huo uligongwa mbele ya:-

…………………………

Julius Ulaya

Mtendaji

Kijiji cha Mgansa

…………………………

Kliford M. Simtuka

Mwenyekiti

Kijiji cha Mgansa

**KUIDHINISHWA:**

Sheria ndogo hizi ziliidhinishwa na halmashauri ya Wilaya ya Mpanda kufuatia mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe ……/……/20…… na muhuri wa halmashauri uligongwa mbele ya:-

…………………

Romuli R. John

Mkurugenzi Mtendaji

Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda

……………………………………

Hamad H. Mapengo

Mwenyekiti

Halmashauri ya Wilaya Mpanda

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

**(SURA 287 TOLEO LA 2002)**

**SHERIA NDOGO**

**(Zimetungwa chini ya kifungu cha 168)**

**SHERIA NDOGO (ADA, MAKOSA NA ADHABU) ZA KIJIJI CHA RUGUFU ZA MWAKA 2018**

Jina 1. Sheria ndogo hizi zitajuliana kama sharia ndogo za kijji cha Rugufu za mwaka 2018.

Matumizi 2. Sheria ndogo hizi zitatumika katika eneo lolote la kijiji cha Rugufu na zitaanza kutumika mara baada ya kuthibitishwa na baraza la madiwani la halmashauri ya wilaya ya Mpanda.

Tafsiri 3. Katika sheria ndogo hizi maneno yafuatayo yatakuwa na maana ifuatayo:-

"Halmashauri" - maana yake halmashauri ya kijiji cha Rugufu.
"kijiji"- maana yake ni kjji cha Rugufu.
"mwanakijiji"- ni mtu yeyote mkazi wa kkijiji cha Rugufu.
"mzazi"- maana yake ni pamoja na mlezi
"mifugo"- maana yakeni ng'ombe, mbuzi, nguruwe, kondoo, kuku, mbwa, na paka.
"mkutano"- maana yake ni mkutano mkuu wa kijiji, kikao cha halmashauri ya kijiji, vikao vya kudumu na mikutano ya vitongoji.
"Afisa mtendaji wa kijiji"- maana yake ni pamoja na kaimu afisa mtendaji wa kijiji.
"shughuli za maendeleo"- maana yake ni shughuli zinazo shughulikiwa na serikali ya kijiji ambazo kila mwaka kijiji ambaye ni mtu mwenye umri wa miaka 18 na Zaidi, isipokuwa mwanafuzi, anatakiwa kushiriki kwa kutoa nguvu zake na fedha.

4. **MAKOSA YANAYOHUSU MAENDELEO NA UTAWALA**

Shughuli za maendeleo.

i

i. Ni kosa kwa mwanakijiji mwenye uwezo wa kufanya kazi na mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea, kutoshiriki katika shughuli za maendeleo. Mwanakijiji atakaye bainika ametenda kosa hilo atatozwa faini ya shilingi elfu tano(5000/=) na kuamriwa kufanya shughuli husika.

ii. Ni kosa kwa mtu yoyote kuingia kwenye taasisi yoyote ya Umma bila idhini au sababu maalum. Atakayebainika ametenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh. 10,000/=

iii. Ni kosa kwa mwanakijiji yeyote kupinga au kutoshiriki shughuli za maendeleo ya kijiji bila sababu za msingi, au kushawishi wanakijiji wengine wasishiriki katika

shughuli za maendeleo, mwanakiiji atakaye tiwa hatiani kwa kosa hili ataadhibiwa kama ifuatavyo:-

i. Endapo ni kosa la kushawishi wanakijiji wengine wasishiriki shughuli za maendeleo ya kijiji faini itauwa Tsh. 20,000/=
ii. Ni marufuku kwa mtu yeyote kupiga mbiu bila idhini ya serikali ya kijiji au mwenyekiti wa kitongoji, faini kwa atakaye kutwa na hatia atalipa faini ya Tsh.10,000/=
iii. Ni marufuku kwa mtu yeyote kubandika vipeperushi vya uchochezi dhidi ya taasisi yoyote ile, atakaye bainika atatozwa faini ya Tsh. 30,000/= na kufikishwa kwenye vyombo vya sharia.
iv. Mwanakijiji atakaye mpokea mgeni bila kutoa taarifa kwa mwenyekiti wa kijiji au kitongoji atatozwa faini ya Tsh.10,000/=
v. Mtu yeyote atakaye zuia mgambo/polisi jamii kumkamata mharifu au kutoa lugha za matusi atakaye bainika atatozwa faini ya Tsh. 30,000/=

**MUDA WA KAZI.**

Kuanzia saa moja na nusu asubuhi mpaka saa tisa alasiri utakuwa muda wa kazi.

Ni marufuku mtu yoyote kuzurura au kunywa pombe muda wa kazi, atakayebainika atakuwa ametenda kosa na atatozwa faini ya Tsh.20,000/=

Ni kosa kufanya shughuli yoyote ya biashara zaidi ya saa nne usiku atakayebainika ataadhibiwakama ifuatavyo:-

i. Endapo ni kosa la uuzaji pombe Zaidi ya muda usioruhusiwa atatozwa faini ya Tsh. 20,000/=
ii. Endapo ni kosa la kuonyesha cinema au kucheza disko atatozw faini ya Tsh. 20,000/=
iii. Ni marufuku kuuza pombe maeneo yasiyoruhusiwa atakayebanika atatozwa faini ya Tsh.30,000/=
iv. Mtu yeyote atakayeuza, lim, pika, aina yoyote ya madawa ya kulevya atatozwa faini ya Tsh.20,000/= na kufikishwa kwenye vyombo vya sharia.
v. Mtu yeyote atakaye vaa nguo za kuonesha maumbile

au nguo zinazo haribu mila za kitanzania atakayebainika atatozwa fainiyaTsh. 20,000/=

vi. Endapo ni biashara ambazo hazikuainishwa katika kifungu hiki faini ni Tsh. 20,000/=

6. **KUTOA LUGHA ZA MATUSI NA VITISHO**

i. Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kutoa lugha za matusi hadharani, mtu atakayebainika kutenda kosa hili atalipa faini ya Tsh. 30,000/=

ii. Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kupigana hadharani, atakayebainika katenda kosa hili atalipa faini ya Tsh. 30,000/=

iii. Ni kosa kumtishia mtu yoyote kwa lugha za vitisho au matendo. Atakayebainika atatozwa faini ya Tsh. 50,000/= na kupewa onyo kali au kufikishwa kwenye mahakamani.

7. **WAJIBU WA KUHUDHURIA MKUTANO WA KIJIJI AU KITONGOJI**

i. Ni wajbu wa kila mwankijiji mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea kuhudhuria mikutano ya kijiji.

ii. Ni kosa kwa mwanakijiji yeyote kutohudhuria katika mkutano wa kijiji bila taarifa ya msingi, na atakaye tenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh. 5000/=

iii. Ni kosa kwa mtu yeyote kuhudhuria kwenye mkutano akiwa na zana za kilmo mf. Panga, kisu, fimbo, au manati. Mtu atakaye tenda kosa hili atatozwa fain ya Tsh. 25,000/=

iv. Ni kosa kwa mtu yeyote kuhudhuria kwenye mikutano ya kijiji akiwa amelewa na kusababisha vurugu. Mtu atakaye tenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh. 25,000/=

8. **KUGOMEA WITO WA VIONGOZI WA KIJIJI.**

i. Ni kosa kugoma wito wa VEO, mwenyekiti wa kijiji au mwenyekiti wa kitongoji.Mtu atakaye tenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh.10,000=

ii. Endapo mwana kijiji atatenda kosa la kulazimika kufuatwa na mgambo atatakiwa kulipa gharama ya kufuatwa na mgambo ambayo ni Tsh. 20,000=

9. **MAKOSA YANAYOHUSU ELIMU NA WATOTO**

i. Kila mzazi atakuwa na wajibu wa kumuandikisha mtoto wake aliyefika umri wa kwenda shule.

ii. Mzazi ambaye atashindwa kumwandikisha mtoto na kuhakikisha kuwa mtoto wake anakwenda shule, mzazi atakayepatikana na hatia hii atatozwa faini ya Tsh. 20,000/= na kuamliwa kumpeleka mtoto shule.

iii. Nikosa kwa mzazi kuacha kununua sare za shule au vifaa vya shule vinavyohitajika kwa ajili ya mtoto wake na mzazi atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh. 10,000/= na kutakiwa kununua vifaa vinavyotakiwa

iv. Mzazi atakayepewa taarfa za utoro wa mwanae na kushindwa kuchuua hatua zozote atakuwa ametenda kosa na faini itauwa Tsh. 20,000/=

v. Mzazi atakayeshindwa kumpeleka mwanafunzi aliyefaulu sekondari atakuwa ametenda kosa na aikutwa na hatia atatozwa faini ya Tsh. 20,000/= na kutakiwa kumpeleka mwanafunzi shule.

vi. Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kumuonyesha mwanafunzi picha za ngono atakayetiwa hatiani atatozwa faini ya Tsh. 50,000/= na kufikishwa mahakamani.

vii. Mtoto akifaulu kwenda sekondari na mzazi hana uwezo wa kumsomesha atoe taarifa kwa mwenyekiti wa kijiji iliaitishe mkutano ili mtoto asaidiwe.

viii. Mtu yeyote atakaye mshawishi mwanafunzi kujihusisha na masuala ya ngono atakuwa ametenda kosa , Atatozwa faini ya Tsh 50,000/= na kufikishwa mahakamani.

ix. Ni kosa mwanafunzi kuzurura ovyo wakati wa masomo darasani bila sababu ya msingi mwanafunzi atakaye tiwa hatiani kwa kosa hili mzaziwake atatozwa faini ya Tsh 10,000/=

x. Ni kosa kumshawishi mwanafunzi afanye vibaya katika mitihani. Atakayebainika atalipa faini ya Tsh. 50,000/=

xi. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuingia gesti , vilabu vya pmbe au dosko za usiku. Mtu yeyote atakayeingia au kuruhusu mwnafunzi kuingia katika sehemu hizo atakuwa ametenda kosa na ataadhibiwa kama

ifuatavyo:-

a. Endapo nikosa la mmiliki kuruusu mwnafunzi kuingia atatozwa faini ya Tsh 50,000/=

b. Endapo I kosa la mtu kuingia na mwanafnzi faini Tsh 50,000=

c. Mwanafunzi atapewa adhabu kali na onyo kali.

10. **KUMWAJIRI MWANAFUNZI**

i. Ni kosa kumwajiri mwanafunzi atakayetenda kosa hili atatozwa faini ta Tsh 50,000/= na kusitisha ajira

ii. Ni kosa kuuajiri mtoto aliechini ya umri wa miaka 14, atakaye bainika ametenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 20,000 na kusitisha ajira.

11. **MAKOSA YANAYOHUSU AFYA NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA**

Itakuwa ni lazima kwa kila kaya kuwa na kichanja, shimo la tak na choo bora kilichojengwa na matofali na kufunikwa pamoja na lango imara. Kaya itakayo bainika imekiuka kifungu hiki itakuwa imetenda kosa itaadhibiwa kama ifatavyo;-

i. Endapo ni kosa la kutokuwa na choo bora au kukosa choo kabisa faini yake ni Tsh 10,000/= na kuamriwa kujenga choo kwa muda uioamriwa na mamalaka husika.

ii. Endapo ni kosa la kutokuwa na kichanja, shimo la taka, kibuyu chilizi. Kaya itatozwa faini ya Tsh 10,000/= na kuamriwa kucimba shimo la taka, shimo la karo kwa muda utakao amriwa na mamalaka husika.

iii. Ni kosa kuoga, kuogesha vyombo au kufuria karibu kisima cha maji au kwenye chanzo cha mto. Mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ta Tsh 20,000/=

iv. Ni kosa kwa mtu yeyote kufanya shughuli za kilmo kwenye hifadhi ya mito, atakaye tenda kosa hili atatozwa faini ya ths 50,000/=

v. Ni kosa kuacha nyumba katika mazingira machafu. Mtu atakaye tenda kosa hii atatozwa faini ya Tsh 10,000/= na kuamriwa kusafisha.

vi. Ni kosa kuuza chakula, pombe katika hali ya uchafu. Mtu atakaye tenda kosa hili atatozwa

faini ta Tsh 10,000/= na biashara yake kufungwa mpaka mazingira yatakapokuwa safi.

vii. Ni marufuku mtu yoyote kujisaidia hadharani, mtu atakaye bainika ametenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 30,000/=

viii. Ni marufuku mtu yeyote kuvua samaki mto Rugufu kwa kutumia sm. Mtu atakayetiwa hatiani atatozwa faini ya Tsh 50,000/= na kufikishwa mahakamani.

ix. Ni marufuku kufanya mavuno kwenye shamba la mtu (kusalala mazao). Mtu atakayebainika ametenda kosa hilo atatozwa faini ya Tsh 30000/=

x. Ni kosa kwa mwanamke kujifungulia nyumbani au mwanaume kuruhusu mke kujifungulia nyumbani. Atakayetiwa hatiani atatozwa faini ya Tsh.30,000/=

12 **KUCHOMA MOTO**

Ni makosa kuchoma moto msitu au pori la kijiji. Mtu atakayetenda kosa atatozwa faii ya Tsh 50000/= na kulipa fidia ya hasara atakayokuwa mesababisha ikiwa ni pamoja na kupanda miti.

13 **MAKOSA YANAYOHUSU MIFUGO NA KILIMO**

i. Ni kosa kuacha mfugo wa aina yoyte kuzurura ovyo katika eneo la kijiji. Atakayebainika ametenda kosa hili atalipa faini ya Tsh. 10,000/= kwa kila ng'ombe na Tsh. 5,000/= kwa mbuzi , kondoo na nguruwe.

iii. Ni kosa kwa mtu yoyote kulisha mifugo yake katika shamba la mtu mwingine au kuacha mifugo yake ikifanya uharibifu katika shamba la mtu mwingine. Atakayebainika ametenda kosa hili atalipa faini ya Tsh. 50,000/= pamoja na kulipa fidia kwa mwenye shamba kulimgana na tathmini itakayofanywa na Afisa kilimo wa eneo husika.

iv. Ni kosa kwa mtu yoyote kuingiza mifugo yake katika eneo la kijiji bila kibali au kufuata utaratibu za uingizaji wa mifugo katika kijiji. Atakayebainika ametenda kosa hili atalipa faini ya Tsh. 50,000/= na kuamriwa kuondoa mifugo yake kijijini.

v. Ni kosa kwa mwanakijiji yoyote kumpokea mfugaji bila

kufuata taratibu zingine za uingizaji mifugo katika kijiji. Atakayebainika ametenda kosa hili atalipa faini ya Tsh. 50,000/= na kuamriwa kumuondosha mfugaji huyo.

vi. Ni kosa kuacha Mbwa wakizurura hovyo. Atakayebainika ametenda kosa hili atalipa faini ya Tsh. 20,000/=

vii. Ni kosa kwa mtu yoyote kuuza nyama isiyokaguliwa na wataalamu wa Afya. Atakayebainika ametenda kosa hili atalipa faini ya Tsh. 20,000/=

viii. Bucha zote ni lazima ziwe na hadhi iliyokubalika kisheria kulingana na taratibu za sheria za vyakula. Atakayekiuka atapewa onyo na kuamriwa kutengeneza bucha.

ix. Ni kosa kupitisha ng'ombe barabarani**.** Atakayebainika ametenda kosa hili atalipa faini ya Tsh. 50,000/=

15 **KILIMO, UJENZI NA ADHABU ZAKE**

i.Mtu yoyote atakayebainika amejenga au kulima katika eneo la kupitisha mifugo atatozwa faini ya Tsh. 50,000/= na kuamriwa kuondoka.

ii. Ni marufuku kwa mtu yoyote kulima au kujenga kwenye barabara za mtaa. Atakayebainika ametenda kosa hili atalipa faini ya Tsh. 50,000/= na kuondolewa.

iii. Ni kosa kulima katika eneo la hifadhi ya kijiji. Atakayebainika ametenda kosa hili atalipa faini ya Tsh. 50,000/= na kuondolewa.

**iv.** Ni kosa kwa mtu yoyote kushindwa kuendeleza uwanja aliopewa na Serikali ya kijiji kwa muda wa miaka mitatu. Atakayeshidwa atanyang'anywa na kupewa mtu mwingine.

16 **ADA NA USHURU MBALIMBALI**

Kijiji kitatoza ada mbalimbali kama ifuatavyo:

i. Ada ya maombi ya zabuni ni Ths. 50,000/=

ii. Ada ya uchimbaji wa madini kwenye kremu ni Tsh. 50, 000/= kwa mwezi

iii. Ada ya kuweka mizinga katika kijiji itakuwa ni Tsh. 2000 kwa kila mzinga.

iv. Serikali ya kijiji itatoza Tsh. 10,000/= kama ushuru wa mauziano husika, kwa muuza nguo, vyombo chakavu, kuonesha sinema itatoza Tsh. 5,000/= kwa siku

v. Ni kosa kwa mtu yoyote kukataa kulipa ada au ushuru.

Atakayetenda kosa hili atalipa faini ya Tsh. 20,000 na kulipa ushuru au ada husika.

16 Ni kosa kutoa au kupokea fedha kwa ajili ya malipo ya ushuru bila kutoa au kuoewa stakabadhi. Atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh. 5000/= na kutoa/ kupikea stakabadhi.

Muhuri wa Serikali ya kijiji uligongwa kwenye sheria ndogo hizi kufuatia azimio la mkutano mkuu wa kijiji uliofanyika tarehe ……………….. na muhuri huo uligongwa mbele ya:-

…..........................
Vith Atanazi
Afisa Mtendaji
Kijiji cha Rugufu

…..........................
Josephat Samwel
Mwenyekiti
Kijiji cha Rugufu

**KUIDHINISHWA:**

Sheria ndogo hizi ziliidhinishwa na halmashauri ya Wilaya ya Mpanda kufuatia mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe ……/……/20…… na muhuri wa halmashauri uligongwa mbele ya:-

…...................
Romuli R. John
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda

….......................................
Hamad H. Mapengo
Mwenyekiti
Halmashauri ya Wilaya Mpanda

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

**(SURA 287 TOLEO LA 2002)**

**SHERIA NDOGO**

**(Zimetungwa chini ya kifungu cha 168)**

**SHERIA NDOGO (ADA, MAKOSA NA ADHABU) ZA KIJIJI CHA MAZWE ZA MWAKA 2018**

| | | |
|---|---|---|
| Jina | 1. | Sheria ndogo hizi zitajulikana kama sharia ndogo Ada makosa makosa na Adhabu za kjiji cha Mazwe za Mwaka 2018 |
| Matumizi | 2. | Sheria ndogo hizi zitatumika mara baada ya kuidhinishwa na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda |
| Tafsiri | 3. | Katika sharia ndogo hizi maneno yafuatayo yatakua na maana kama ifuatavyo:- |
| | | Halmashauri" Maana yake Halmashauri ya Kijiji cha mazwe |

Kijiji " Maana yake ni kijiji cha Mazwe
Mwanakijij i" Maana yake ni yeyote mkazi wa kijiji cha Mazwe
Mzazi " Maana yake ni pamoja na mlezi
Mifugo " Maana yake ni ng`ombe, mbuzi, kondoo, nk
" Mkutano " Maana yake ni Mkutano Mkuu wa Kijiji vikao vya kudumu na mkutano wa kitongoji

4. ADA MBALIMBALI

i) Ada ya Maombi ya zabuni itakua 50,000/= kwa kila zabuni moja kutegemeana na mradi wenyewe
ii) Serikali ya kijiji itatoza ada ya Tsh 10,000/= ya kushuhudia watu wanaposaini Mikataba mbalimbali isipokua mikataba ya ujenzi wa miradi ya maendeleo

5. MAKOSA YA KIUTAWALA

Itakuwa ni kosa kwa mwanakijiji yeyote kufanya yafuatayo

i) Kukataa kushiriki shughuli ya maendeleo ya kijiji, mtu yeyote atakayetenda kosa hili akikutwa na hatia atatozwa faini ya Tsh 10,000/= na kuariwa kushiriki.
ii) Kukataa kuchangia Mchango wa Maendeleo Kijijini. Mtu yeyote atakayetenda kosa hili akikutwa na hatia atatozwa faini ya Tsh 10,000/= na kuamriwa kutoa mchango husika
iii) Mjumbe/Mwanakijiji kushindwa kuhudhuria Mkutano wa kijiji au Kitongoji bila sababu ya msingi. Mtu yeyote atakayetenda kosa hili akikutwa na hatia atatozwa faini ya Tsh 5,000/=
iv) Mwenyekiti wa kitongoji kutokualika mkutano atatozwa faini ya Tsh 10,000/=
v) Mjumbe kuchelewa kikaoni atatozwa faini ya Tsh 2,000/=
vi) Mwanakijiji kupokea mgeni na kushindwa taarifa kwa balozi, M/kiti wa kijiji au kitongoji atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 10,000/=
vii) Kutukana hadharani mtu atakayebainika ametenda kosa kulingana na kifungu hiki atatozwa faini ya Tsh 50,000/= kwa kila mhusika
viii) Kupigana hadharani mtu atakayebainika ametenda kosa kulingana na kifungu hiki atatozwa faini ya Tsh 50,000/= kwa kila mhusika
ix) Kutofanya kazi ( Uzembe) na kuzurura saa za kazi kuanzia saa1:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana na zaidi ya saa6:00 usiku, Mtu atakayebainika kutenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 10,000/=
x) Mtu yeyote atakayekutwa amevaa nguo za aibu za ndani na kuonyesha maungo ya ndani akikutwa na kosa hilo atatozwa faini ya Tsh 20,000/=
xi) Kuendesha pikipiki na baiskeli kwenye njia ndogo za kuingia ndani ya soko na kutoka faini ni Tsh 5,000/=
xii) Kucheza disko/video nje ya muda ulioruhusiwa mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 50,000/= kwa mshiriki wa mziki/ukumbi ni Tsh 10,000/= kwa mchezaji

xiii) Kuishi maeneo yasiyo ya makazi, Mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 20,000/=

xiv) Kunywa pombe na kuuza pombe saa za kazi na usiku zaidi ya saa sita mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 50,000/=

xv) Kugomea au kukaidi wito wa afisa mtendaji wa kijiji au mwenyekiti wa kijiji au kitongoji mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 10,000/=

xvi) Kutoa tangazo au kupiga mbiu bila idhini ya serikali ya kijiji, Mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 10,000/=

xvii) Atakayebandua tangazo lililobandikwa atatozwa Tsh 10,000/=

6. MAKOSA YA KIELIMU NA ADHABU ZAKE

Mtu yoyote atakayefanya matendo yafuatayo atakuwa ametenda kosa na akikutwa na hatia ataadhibiwa kama ifuatavyo:

i. Mzazi kushindwa kumwandikisha shule mtoto aliyefikia umri wa kwenda shule atatozwa faini ya Tsh. 20,000/= na kuamriwa kumwandikisha.
ii. Mzazi kushindwa kumdhibiti mwanafunzi kwenye utoro wa zaidi ya siku tano atatozwa faini ya Tsh.10,000/= na onyo kali
iii. Mzazi kuacha kumnunulia mwanafunzi sare za shule bila sababu ya msingi ikiwa ni pamoja na vifaa vya kujifunzia atatozwa faini ya Tsh. 5,000/= na kuamriwa kununua sare/ vifaa hivyo.
iv. \Kumwajiri mwanafunzi muda wa masomo faini itakuwa Tsh. 20,000/= na kusitisha ajira husika.
v. Mmiliki wa baa au disko kumruhusu mwanafunzi kuingia ndani ya baa au disko atatozwa faini ya Ths. 10,000/=
vi. Mzazi kuacha kumpeleka mwanafunzi aliyefaulu shule ya sekondari atatozwa faini ya Tsh.50,000/= na kumpeleka shuleni.
vii. Kwenda kwenye Taasisi ya Elimu/Umma bila shida au sababu maalum atatozwa faini ya Tsh. 10,000/= na kufanya shughuli nyingine yoyote katika eneo la ofisi.
viii. Kumwonyesha video ya ngono mwanafunzi, atakayebainika atatozwa faini ya Tsh.50,000/=
ix. Mzazi kumtuma mwanafunzi kuuza pombe kilabuni atatozwa faini ya Tsh. 50,000/=
x. Atakayebainika kumshawishi Mwanafunzi tofauti na maadili yake ya shuleni atatozwa faini ya Tsh. 50,000/=
xi. Mzazi ayakayemshawishi mwanafunzi kufanya vibaya kwenye mitihani ya shule atatozwa faini ya Tsh. 50,000/=.

7. **MAKOSA NA ADHABU YA KILIMO NA MIFUGO**

Mtu atakayetenda yafuatayo atakua ametenda kosa ataadhibiwa kama ifuatavyo

i) Kuchungia mifugo maeneo yasiyoruhusiwa, Mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 50,000/=

ii) Mifugo kuharibu mazao ya mtu, Mwenye mifugo atatozwa faini ya Tsh 25,000/= na kulipa fidia kwa kwenye mazao kwa kuzingatia tathmni ya uharibifu itakayofanywa na Afisa kilimo wa eneo husika

iii) Kulima eneo lisiloruhusiwa au lililohifadhiwa, Mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 50,000/=
iv) Kulima au kujenga katika njia za mifugo ndani ya mita (15), Mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 50,000/= na kuondolewa eneo husika
v) Kufuga ng`ombe kwenye vyanzo vya maji faini ni Tsh 50,000/=
vi) Mtu atakayeachia mbuzi na kondoo wakati wa kiangazi bila ya kuzichunga atatozwa faini Tsh 10,000/=

Kwa mfugaji wa mbwa ambaye hatochanjisha mbwa wake na kumwacha na akazurule ovyo atatozwa faini ya Tsh 10,000/=

8. MAKOSA NA ADHABU YANAYOHUSU AFYA

Itakua ni kosa

i) Kaya kutokua na choo, Kaya itakayopatikana na kosa hili atatozwa faini ya Tsh 10,000/= na kuamriwa kuchimba choo
ii) Kaya kutokua na karo, kichanja na shimo la taka, Kaya itakayotenda kosa hili itatozwa faini ya Tsh 2,000/= na kuamriwa kutengeneza
iii) Kuacha mazingira ya nyumba katika hali ya uchafu, Mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 10,000/= na kuamriwa kusafisha
iv) Kuoga na kufulia nguo kwenye kisima cha maji na mto ndani ya umbali wa mita (10) kutoka kwenye kisima au mto, Mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 20,000/=

9. **MAKOSA NA ADHABU YA KILIMO NA MAZINGIRA**

Mtu yeyote atakayekua ametenda makosa yaliyoainishwa hapa chini ataadhibiwa kama ifuatavyo

i) Kulima/ kukata miti au kuchungia mifugo kwenye chanzo cha maji, Mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 50,000/=
ii) Kuchoma moto bila kuchukua tahadhari na kusababisha kuunguza pori, Mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 50,000/=
iii) Kufyeka msitu uliohifadiwa, Mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 50,000/= na kuamriwa kupandamiti
iv) Kulima ndani ya hifadhi ya barabara kuu au mtaa, Mtu atakayetenda kosa hili atatozwa faini ya Tsh 25,000/=

Muhuri wa Serikali ya kijiji uligongwa kwenye sheria ndogo hizi kufuatia azimio la mkutano mkuu wa kijiji uliofanyika tarehe ……………….. na muhuri huo uligongwa mbele ya:-

…..……………………
Edward M. Nyabenda.
Katibu wa kijiji
Kijiji cha Mazwe

…..……………………
Msonera M. Saimon
Mwenyekiti

Kijiji cha Mazwe

**KUIDHINISHWA:**

Sheria ndogo hizi ziliidhinishwa na halmashauri ya Wilaya ya Mpanda kufuatia mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe ……/……/20…… na muhuri wa halmashauri uligongwa mbele ya:-

…………………
Romuli R. John
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda

………………………………………

Hamad H. Mapengo
Mwenyekiti
Halmashauri ya Wilaya Mpanda

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

**(SURA 287 TOLEO LA 2002)**

**MAPENDEKEZO YA SHERIA NDOGO**

**(Zimetungwa chini ya kifungu cha 168)**

**SHERIA NDOGO (KUSIMAMIA MSITU WA HIFADHI WA NTAKATA) ZA KIJIJI CHA LUGONESI ZA MWAKA 2018.**

| | | |
|---|---|---|
| *Jina* | 1. | Sheria hii inaitwa Sheria ndogo ya Kijiji cha LUGONESI ya Kusimamia Msitu wa hifadhi wa NTAKATA iliyotungwa chini ya kifungu Na. 168 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Na. 7 ya mwaka 1982 na itasomwa pamoja na Rasimu ya Mpango wa usimamizi wa msitu wa Hifadhi wa NTAKATA kijiji cha LUGONESI. |
| *Matumizi* | 2. | Sheria hii itatumika katika mipaka ya eneo lote la kijiji cha LUGONESI na itaanza kutumika mara itakapoidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda. |
| *Tafsiri* | 3. | Katika sheria ndogo hizi maneno yafuatayo yatakuwa na |

maana kama ifuatavyo: -

"**Halmashauri"** maana yake ni Halmashauri ya kijiji cha LUGONESI.

**"Dawa za asili"** maana yake ni dawa za miti shamba

**"Doria"** maana yake ni kuzunguka maeneo ya msitu kwa lengo la kukagua kunakofanywa na kikosi maalum cha doria.

**"Kamati"** maana yake ni Kamati ya Huduma za jamii Mazingira ya kijiji cha LUGONESI.

**"Kuni"** maana yake ni miti iliyokauka na kudondoka.

**"Leseni"** maana yake ni kama ilivyoainishwa kwenye rasimu ya mpango wa usimamizi wa msitu wa hifadhi ya NTAKATA.

**"Mifugo"** maana yake ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda, mbwa na nguruwe.

**"Kijiji"** maana yake ni kijiji cha Lugonesi

**"Msitu"** maana yake ni Hifadhi ya msitu wa NTAKATA

**"Mtendaji wa kijiji"** maana yake ni Mtendaji wa kijiji cha LUGONESI aliyepo kisheria.

**"Mwanakijiji"** maana yake ni mkazi wa kijiji cha LUGONESI

"**Rasilimali"** maana yake ni mazao ya hifadhi ya msitu wa NTAKATA

**"Mazao ya msitu"** maana yake ni mbao, kuni, dawa za asili na mazao yote yanayopatikana kwenye misitu.

**"Ulinzi"** maana yake ni kulinda rasilimali za hifadhi ya msitu

**"VFR"** maana yake ni Village Forest Reserve/ Hifadhi ya msitu wa kijiji cha LUGONESI

**"VNRC"** maana yake ni Village Natural Resources Committee/ Kamati ya Huduma za jamii na Mazingira ya kijiji cha LUGONESI.

*Kuanzishwa hifadhi ya msitu*

4 Kunaanzishwa hifadhi ya msitu wa NTAKATA unaomilikiwa na kijiji cha LUGONESI.

| | | |
|---|---|---|
| *Usimamizi* | 5. | Msitu utasimamiwa na Kamati ya Huduma za jamii na Mazingira ya Kijiji kwa niaba ya halmashauri ya kijiji na wanakijiji wote wa LUGONESI. |
| *Ulinzi wa msitu* | 6. | Kikosi cha doria kitakuwa ni mlinzi wa msitu wakishirikiana na wananchi wa Kijiji cha Lugonesi. |
| *Madhumuni* | 7. | Lengo na madhumuni ya kuanzisha hifadhi ya msitu huu ni kutunza rasilimali zinazopatikana katika msitu na kuipa kamati ya Huduma za jamii na Mazingira ya kijiji uwezo wa kisheria wa kusimamia Msitu na kuwajibika katika kulinda na kuweka taratibu za kutumia rasilimali zilizomo katika Msitu huu katika msingi endelevu na kutoa adhabu kwa watu watakao kiuka sheria hii, pamoja na taratibu zilizotolewa chini ya sheria hii. |
| *Matumizi* | 8. | Msitu huu utakuwa wa hifadhi lakini unaweza kutumika kwa shughuli zifuatazo kwa kibali cha kamati ya Huduma za jamii na mazingira ya kijiji. |

a) Urinaji wa asali
b) Uchimbaji wa dawa za asili
c) Kuokota kuni
d) Kukata nyasi
e) Kuokota uyoga
f) Kufanya shughuli za matambiko kwa wanakijiji.
g) Utafiti
h) Utalii
i) Uvunaji wa hewa ya ukaa
j) Kukata fito zisizozidi 10 tu.

| | | |
|---|---|---|
| *Makosa* | 9 | Itakuwa ni kosa kufanya yafuatayo katika msitu wa hifadhi |

a) Kuchunga mifugo msituni.
b) Kuingia katika msitu bila kibali
c) Kuchoma mkaa
d) Kukata miti bila Leseni
e) Kuchimba dawa za asili bila kibali
f) Kuokota kuni bila kibali
g) Kufanya shughuli za kilimo
h) Kuchoma moto
i) Kurina asali bila kibali
j) Kufanya makazi
k) Kufanya shughuli nyingine yoyote isiyohusika katika msitu

| | | |
|---|---|---|
| *Makosa mengine* | 10 | Makosa mengine na adhabu zake ni kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, Sheria ya Misitu Na 14 ya mwaka 2002 pamoja na Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009. |
| *Adhabu* | 11 | Mtu yoyote atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa lolote lililoidhinishwa katika kifungu cha 10 cha sheria ndogo hizi ataadhibiwa kama ifuatavyo: |

a) Kosa la kuingiza na kuchunga mifugo atatozwa Tsh 10,000/= kwa kila mbwa, Tshs 5000/= kwa kila ng'ombe na Punda na Tsh 2500/= kwa mbuzi na kondoo. Atakayeshindwa kulipa mifugo yake itaifishwe kulingana na gharama ya faini.
b) Kosa la kuingia msituni bila kibali adhabu yake itakuwa ni faini isiyopungua Tsh 10,000/= na isiyozidi Tsh 50,000/=
c) Kosa la Kuchoma mkaa faini shilingi Tsh 50,000/= na kutaifisha mkaa huo.
d) Kosa la Kukata miti bila kibali adhabu itatolewa kulingana na thamani ya mti uliokatwa na faini isiyopungua Tsh 5,000/= na isizidi Tsh 50,000/= pamoja na kutaifisha miti hiyo.
e) Kosa la Kufanya shughuli za kilimo faini shilingi elfu hamsini (50,000/=) kwa hekari moja, kutaifisha

mazao na kupelekwa mahakamani pale itakapobidi.

f) Kosa la Kuchoma moto faini ya isiyopungua Tsh 20,000/= na isiyozidi Tsh 50,000/= na fidia ya uharibifu.
g) Kosa la Kufanya shughuli nyingine yoyote isiyohusika katika msitu huo atatozwa faini Tsh 30,000/= na fidia pale inapobidi kulingana na sharia husika.
h) Kufanya doria zisizo na taarifa kwa manufaa binafsi faini isiyopungua 20000/= na isiyozidi 50,000/= pamoja na kufukuzwa katika kikosi cha doria au kupelekwa mahakamani inapobidi.

*Mamlaka ya Kamati ya Huduma za jamii na mazingira*

12 Kamati ya Huduma za jamii na mazingira ya kijiji itakuwa na mamlaka kama ifuatavyo

*a)* kumtoza mhalifu gharama zilizotumika wakati wa kumkamata
b) kumtoza fidia mhalifu kwa rasilimali alizovuna kinyume cha sheria
c) Kumuamuru mtuhumiwa au mhalifu kufanya kazi za kijamii kama kusafisha mipaka ya msitu, kupanda miti, kulima barabara kulingana na kosa alilolitenda.
d) Kuwajibisha kikosi cha doria pale inapoona inafaa.
e) Kuhudumia askari wa doria watakaoumia wakiwa kazini kulingana na uwezo wa Kijiji na pesa itakayokuwepo.

f) Kutoza eneo maalumu kwa ajili ya kambi za asali.

*Mgawanyo wa Mapato*

13 Mapato yatakayopatikana kutokana na faini, mauzo ya mazao yaliyokamatwa na vyanzo vingine vinavyotokana na mazao ya msitu huu yatagawiwa na kutumika kama ifuatavyo:

a) Asilimia 50% itatumika kwa ajili ya maendeleo ya kijiji.

b) Asilimia 25% itatumika kwa ajili ya shughuli za uhifadhi ya msitu
c) Asilimia 25% itatumika kuboresha Kamati ya Huduma za jamii na mazingira ya kijiji kwa
   i. Kutoa zawadi kwa Askari wa doria pale inapobidi.
   ii. Kutoa motisha kwa Kamati ya Huduma za jamii na mazingira ya Kijiji
   iii. Kugharamia sare za Askari wa doria
   iv. Kununua zana kwa ajili ya doria
   v. Kugharamia mahitaji wakati wa doria

*Kuanzishwa kikosi cha doria na sifa za mwanakikosi*

14 Kutaanzishwa kikosi cha doria kitakachoundwa na jumla ya watu wasiopungua kumi na mbili wenye sifa zifuatazo:-

a) Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi 45
b) Awe mkazi wa kijiji cha LUGONESI
c) Awe amepitia mafunzo ya VGS/mgambo
d) Awe na uelewa wa msitu
e) Awe tayari kupatikana wakati wowote wa kazi
f) Awe muadilifu, muaminifu na jasiri

*Utaratibu wa matumizi halali ya mazao ya msitu*

15 Ufuatao utakuwa ni utaratibu wa kufuata ili kuhalalisha matumizi ya mazao ya misitu

a) Kuomba kibali au Leseni kwa Mtendaji wa kijiji au mamlaka husika.
b) Kutoa taarifa kwa Mtendaji wa kijiji.
c) Kufanya malipo ya vibali au leseni vinavyotolewa pale inapobidi.
d) Malipo yoyote yatakayofanyika kwenye kijiji ni lazima yakatiwe stakabadhi ya Serikali.
e) Vibali vyote vitatolewa kwa malipo ya Tsh. 1000/= kwa shughuli zote zitakazohitaji kibali. Kibali kitadumu kwa muda wa siku saba (7) wakazi, Tsh. 30,000/= kwa wageni.

*Shughuli zinazohitaji vibali na tozo*

16 Shughuli zifuatazo zitatozwa

| | | |
|---|---|---|
| *kwa kila shughuli* | | a) Kuokota uyoga itakuwa bure<br>b) Kuchimba dawa Tsh. 2000 kwa kila aina ya dawa kwa mkazi na Tsh 10,000 kwa asiye mkaazi.<br>c) Kukata Boriti kwa ajili ya kuezekea Tsh. 500/= kwa kila boriti<br>d) Kukata nyasi kwa ajili ya kuezekea Tsh. 1000/= kwa kila mzigo<br>e) Kuokota kuni Tsh. 500/= kwa matumizi ya nyumbani na Tsh.5000/= meta moja kwa matumizi mengine na Tsh 3000/= kwa meta moja kwa wageni. |
| *Kiongozi wa kikosi cha doria, majukumu na mipaka ya kikosi* | 17 | Kutakuwa na kiongozi wa Kikosi cha doria ambaye atateuliwa na kamati (VNRC) na kuthibitishwa na serikali ya kijiji<br>a) Doria zitapangwa na kuonyeshwa katika mpango kazi wa kamati na kutakuwa na doria kubwa, ndogo, dharula na, maalum<br>b) Mali na watu / watuhumiwa watakaokamatwa wakati wa doria zikabidhiwe kwa kamati/serikali ya kijiji kwa hatua zaidi.<br>c) Askari wa kikosi cha doria hawataruhusiwa kuwapiga watuhumiwa.<br>d) Askari wa kikosi cha doria hawataruhusiwa kutoza faini ya aina yoyote.<br>e) Doria kubwa itafanywa kila baada ya miezi mitatu. |

Muhuri wa Serikali ya kijiji uligongwa kwenye sheria ndogo hizi kufuatia azimio la mkutano mkuu wa kijiji uliofanyika tarehe ………… na muhuri huo uligongwa mbele ya: -

……………………………….

Deodatus P. Kalolo

Afisa Mtendaji

Kijiji cha Lugonesi

……………………………………………

Peter N. Lyakongo

Mwenyekiti Halmashauri ya

Kijiji cha Lugonesi

**KUIDHINISHWA:**

Sheria ndogo hizi ziliidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda kufuatia mkutano wa baraza la madiwani uliofanyika tarehe ……………………… na muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda uligongwa mbele ya: -

…………………………

Romuli R. John

Mkurugenzi Mtendaji
Halmshauri ya Wilaya ya Mpanda

…………………………

Hamad Mapengo

Mwenyekiti

Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

**(SURA YA 287, 2002)**

**ZIMETUNGWA CHINI YA KIFUNGU NAMBA (168)**

**MAPENDEKEZO YA SHERIA NDOGO ZA KUSIMAMIA MPANGO WA MATUMIZIBORA YA ARDHI NA RASILIMALI ZA KIJIJI CHA SIBWESA ZA MWAKA 2018.**

| | | |
|---|---|---|
| Jina | 1. | Sheria hizi zitaitwa sheria ndogo za kusimamia mpango wa matumizi bora ya ardhi na rasilimali za kijiji cha Sibwesa. |
| Tafsiri ya maneno | 2. | Tafsiri ya maneno yaliyotumika kwenye sheria hii<br>**"Serikali ya kijiji"** maana yake ni Halmashauri ya kijiji cha Sibwesa, iliyoundwa chini ya Sheria ya Serikali za mitaa (Mamlaka za wilaya)<br>**"Mkutano Mkuu wa kijiji"** Maana yake ni mkutano wa wanakijiji wa Sibwesaunaoitishwa na kuendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya serikali za mitaa (Mamlaka za Wilaya)<br>**"Kamati ya usimamizi wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji"** Maana yake ni kamati iliyoundwa na halmashauri ya kijiji kuisaidia kazi yake ya usimamizi wa matumizi ya ardhi ya kijiji.<br>**"Kamati ya maji"** Maana yake ni kamati iliyoundwa na halmashauri ya kijiji kusaidia kazi ya usimamizi na uhifadhi wa vyanzo vya maji<br>**"Makazi"** Maana yake ni maeneo yanayokaliwa na watu kwa kujengwanyumba za kuishi au biashara. Katika maeneo haya pia kuna mazao ya kilimo, miti na ufugaji wa ndani<br>**"Kilimo"** Maana yake ni maeneo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Pia nyumba za makazi mtawanyiko<br>**"Huduma za jamii"** Maana yake ni eneo la huduma za jamii kama vile shule, afya (zahanati), barabara, ibada na |

taasisi nyingine

**“Misitu”** Maana yake ni mkusanyiko wa nyasi, miti, vichakavinene na vyembambavyenyeuoto wa asili na miti ya kupandwa kwa matumizi mbalimbali na maeneo mengine yaliyotengwa kama hifadhi ya msitu.

**“Vyanzo vya maji”** Maana yake ni chemichemi, mito, visima, mabwawa, na mabondeyenye maji.

**“Mifugo”**Maana yake ni ng’ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, punda, na kondoo.

**“Mwanakijiji”** Maana yake ni mkazi wa kijiji cha Sibwesa.

**“Mtendaji wa kijiji”** Maana yake ni Afisa Mtendaji wakijiji aliyepo kisheria.

**“Kijiji”** Maana yake ni kijiji cha Sibwesa.

Adhabu zitakazotolewa 3. Sheria hizi zinatoa adhabu ya faini ya kuanzia Shilingi Elfu Moja (1,000/=) mpaka Elfu Hamsini (50,000/=) na kulipa fidia pale inapobidi.

Rasilimali 4 Rasilimali zitakazohusika ni makazi, kilimo, misitu, vyanzo vya maji, malisho ya mifugo,Wanyamapori, madini na nyinginezo.

5 **ENEO LA MAKAZI**

i. Ni kosa kulima au kufanya uharibifu wa aina yoyote ndani ya eneo la barabara. Mtu akibainikaametenda kosa hili, adhabu yake ni faini ya Shilingi Elfu ishirini (20,000/=) na kuzuiwaasiendelee na kilimo.

ii. Kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi, atalazimikakushiriki shughuli zote za maendeleo ikiwemoile ya kutengeneza barabara za kijji pale anapohitajika kufanya hivyo. Mtu atakayevunja sheria hii, adhabu yake ni Shilingi Elfu tano (5,000/=) na kwendakushiriki shughuli aliyopangiwa.

iii. Kila kaya, inalazimika kutunza mazingira yote ya kiwanjachake kwa ujumlaikiwa ni pamoja na eneo la barabara lililombele ya kiwanja mtu akivunja sheria hii atatozwa faini ya Shilingi Elfu tano (5,000/=) na kusafisha maeneo ya mazingira yake

iv. Kila mtu analizimika kutunza alama za mipaka ya kiwanjachake, mtu atakayeharibualama hizi atakuwaametenda kosa. Adhabu ni faini ya Shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) na kuzirudishaalama hizo

v. Ni kosa, kwa mtu yeyote kuharibu mti, kuchuma matunda kwenye mji, bustani bila idhini ya mwenye mali. Mtu akibainikaametenda kosa hili adhabu yake ni Shilingi Elfu Hamsini(50,000) na kulipa fidia.

vi. Ni kosa kuharibu au kusababisha uharibifu wa nyumba ya mtu mwingine kwa namnayeyoteiwe kwa kuchoma moto au kubomoa. Mtu akivunjasheria hii atakuwaametenda kosa. Adhabu yake ni faini ya Shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) na kufidia uharibifu alioufanya.

Kila mtu anayefuga mbwa akimwachia mbwa wake

vii. kuzururaovyo na kusababishamadhara kwa binadamu au mali yake mwenye mbwa atakuwaametenda kosa adhabu Shilingi Elfu Hamsini (50,000) na kugharamiamatibabu au madharayaliyosababishwa na mbwa au kulipa fidia uharibifu huo

viii. Ni kosa kuacha mifugo ikizurura katika eneo la makazi (ng'ombe, mbuzi, kondoo na nguruwe). Mtu atakayevunja sheria hii atatozwa faini ya Shilingi Elfu moja (1,000/=) kwa kila mfugopamoja na kulipa fidia ya uharibifu utakayosababishwa na mifugo hiyo.

ix. Ni kosa kwa wafugajikutokanje ya kijiji kuingiza mifugo kijijini bila kibali halali cha kusafirisha mifugo. Atakayebainika kufanya hivyo atatozwa faini ya Shilingi Elfu Kumi kwa kila ng'ombe (10,000/=) na Shilingi Elfu tano kwa mbuzi na kondoo pamoja na kurudimahalialipotoka.

x. Kila mfugajiatalazimikakuwa na mifugo aina ya ng'ombe wasiozidiishirini (20) katika eneo la makazi (zero grazing) wakati wa msimu wa kilimo. Endapoidadi hiyo itazidibasimfugajiatalazimikakuwapeleka kwenye eneo lililotengwa kwa shughuli za ufugaji. Atakayekiuka atatozwa faini ya Tsh.
Elfu hamsini (50,000/=)

6 **ENEO LA KILIMO**

i. Ni kosa kuvuna mazao kwenye shamba la mtu mwingine

bila idhini ya mwenye shamba. Atakayebainika kuvunja sheria hii, adhabu yake ni faini ya Shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) na kulipa fidia

ii. Ni kosa kusafisha shamba kwa kuchoma moto atakayesafisha kwa kuchoma moto atakuwaametenda kosa na adhabu yake ni Shilingi Elfu hamsini (50,000/=) na kulipa fidia kwa uharibifu utakaojitokeza.

iii. Kila mtu analazimika kutunza alama za mipaka ya shamba lake, mtu atakayeharibu au kujiongezeaalama hizi atakuwaametenda kosa. Adhabu ni faini ya Shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) na kulazimikakurudishaalama hizo

iv. Ni kosa kufanya njiakatikati ya shamba la mwingine. Atakayebainika atatozwa faini ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) na kulipa fidia.

v. Ni kosa kulishamifugo kwenye shamba la mtu mwingine. Atakayebainika atatozwa faini ya Tsh. 10,000/= kwa kila mfugo na fidia.

**ENEO LA MISITU**

7 i. Ni kosa kuingia katika eneo la hifadhi ya msitu wa kijiji wa matumizi na kukata miti bila kibali. Shughuli za ujenzi, kulima, kuishi, kukoboa magome au kuchimbamashimohazitoruhusiwa. Atakayevunja sheria hii atatozwa faini ya Shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) nakusitisha shughuli hizo.

ii. Ni kosa kubangua magome ya miti kwa shughuli yeyote bila kibali, Atakayebainika atatozwa faini shilingi Elfu Kumi (10000/=) na kulipa fidia kulingana na thamani ya mti husika.

iii. Ni kosa kuchoma moto katika maeneo ya msitu wa kijiji. Mtu atakayevunja sheria hii adhabu yake ni kulipa faini ya Shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) na kufidia uharibifu uliojitokeza.

iv. Ni kosa kuvuna miti ambayoimehifadhiwa kisheria katika misitu ya hifadhi ya kijiji au maeneo huria. Mtu akivunja sheria hii, atakuwaametenda kosa. Adhabu yake ni faini ya Shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) na kutaifishwa /kunyang'anywa mbao/mti.

v. Ni kosa kuingiza mifugo kwenye eneo la hifadhi ya misitu ya kijiji bila idhini ya mamlaka husika. Mtu akivunja sheria hii, adhabu yake ni kulipa faini ya Shilingi Elfu Hamsini Tshs (50,000/=).

vi. Ni kosa kuvuna mazao ya misitu au kuwinda wanyama bila kibali. Mtu akivunja Sheria atahukumiwa kwa mujibu wa Sheria ya Misitu na Sheria ya Wanyamapori.

8 **MAENEO YA VYANZO VYA MAJI**

i. Ni kosa kufanya shughuli za kuoga, kulima na adhabu yake ni shilingi Elfu tano(5000/=) au kung'olewa mazao yake, pia kunawa, kujisaidia, kufulia na kuosheavyombo ndani ya Mita thelathini (30M) kwenye maeneo ya vyanzo

vya maji kama mitomidogo na umbali wa Mita Sitini (60M) kwenye maeneo ya Mito Mikubwa. Atakayevunja sheria hii atatozwa faini ya Shilingi Elfu Kumi (10,000/=)

ii. Ni kosa kukata miti, kujenga, kulima, kunywesha mifugo, kuchafua kwa namna yoyote ile kwenye vyanzo vya maji. Atakayevunja sheria hii atatozwa faini ni ya Shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) na kurudisha eneo katika hali yake ya awali kwa kupanda miti rafiki ya maji.

9 **MAENEO YA MALISHO YA MIFUGO**

i. Ni kosa kuchoma moto eneo la malisho ya mifugo. Mtu atakayevunja sheria hii atatozwa faini ya Shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) na kufidiauharibufu na hasara iliyotokea.

ii. Ni kosa kuwa na mifugo inayozidi uwezo wa maeneo ya malisho yalitengwa, kama mifugo itazidiwafugajiwalazimikekupunguza kwa kufuata utaratibu utakaowekwa na mamlaka ya kijiji. Mtu atakayeshindwakutekeleza sheria hii serikali ya kijiji italazimika kusimamia upunguzaji wa mifugo yake kwa kuiuza na fedha itakayopatikanaatakabidhiwamwenye mifugo baada ya kukata gharama ya uendeshaji wa zoezi la uuzaji na usumbufu.

iii. Ni lazima kila mwenye mifugo kuchanja na kuogesha mifugo yake ili kudhibitikuenea kwa magonjwaambukizi. Mtu atakayekiuka utaratibu huu atatozwa faini ya Shilingi Elfu Kumi (10,000/=) kwa kila ng’ombe na kuchanja au

kuogesha mifugo yake pindiamalizapo adhabu.

iv. Ni kosa kwa mfugajikuchungia mifugo katika maeneo yaliyotengwa kwa matumizi mengine. Atakayevunja sheria hii atatozwa faini ya Shilingi Elfu kumi (10,000/=) kwa kila ng’ombe na kulipa fidia.

v. Ni kosa kulima au kuendesha shughuli za aina yeyotezinazoweza kuharibu ubora wa malisho ya mifugo. Mtu atakayevunja sheria hii atatozwa faini ya Shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) na mazao yake yatalishwa mifugo.

vi Kila mfugajianatakiwakuwa na ziziimara la mifugo yake, Atakayekaidikujengazizi atatozwa faini ya Shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) na kujengazizi.

**MAENEO YAHUDUMA ZA JAMII**

10 i. Ni kosa kufanya shughuli zilizo kinyume na matumizi ya maeneo huduma za jamii. Mtu yoyote atakayekiuka atatozwa fain ya Tsh. 10,000/= na kuamriwakusitisha shughuli hiyo

ii. Kila mwananchiatalazimika kufuata taratibu zilizoweka katika maeneo ya huduma za jamii. Atakayekaidiatakuwaametenda kosa na atatozwa faini ya shilgin Elfu kumi (10,000/=)

iii. Maeneo yote ya huduma za jamiiyatatumika kama yalivyopangwa, matumizi yatabadilika kwa idhini ya serikali ya kijiji.

**MAENEO YA MATAMBIKO**

11 i. Ni kosa kufanya shughuli yoyote ndani ya mita sitini (60M) kwenye eneo la matambiko. Atakayekiuka atatozwa faini ya shilingi elfu hamsini (50,000/=)

ii. Kibali cha kufanya shughuli za matambiko kitatolewa na Chifu wa eneo.

**MAENEO YA MAPALILO**

12 i. Ni kosa kuchimbamashimo au kulima au kufanya shughuli yoyote kwenye eneo lililotengwa kwa ajili ya mapitio ya mifugo. Atakayekiuka atatozwa faini ya shilingi Elfu hamsini (50,000/=) na kusitisha shughuli hizo.

ii. Ni kosa kufanya shughuli yoyote iliyo kinyume na matumizi ya palilo.

Muhuri wa Serikali ya kijiji uligongwa kwenye sheria ndogo hizi kufuatiaazimio la Mkutano Mkuu wa kijiji uliofanyikatarehe ……………… 2018 na muhuri huo uligongwambeleya:-

……………………….
Regina M. Jonas
Afisa Mtendaji,
Kijiji cha Sibwesa.

………………………..
Makoye M. Kumba
Mwenyekiti,
Halmashauri ya Kijiji cha Sibwesa.

**KUIDHINISHWA:**

Sheria ndogo hizi ziliidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda kufuatia mkutano wa baraza la madiwani uliofanyikatarehe …………2018 na muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda uligongwa mbeleya:-

…………………
Romuli R. John
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
Mpanda.

……………………..
Hamad H. Mapengo
Mwenyekiti,
Halmashauri ya Wilaya,
Mpanda